https://dspace.org/

# Darasa Za Kimaharajani Za Nyakanga-Kungwi-Sheikh Juma Amiri Kuhusu Unyumba

**Karama, Mohamed**

**2019**
Jarida la Afrika Mashariki la Masomo ya Kiswahili
http://ir-library.kabianga.ac.ke/handle/123456789/416
Karama, M. (2019). Darasa za Kimaharajani za Nyakanga-Kungwi-Sheikh Juma Amiri Kuhusu Unyumba. Jarida la Afrika Mashariki la Masomo ya Kiswahili, 1(4), 129-141.

Downloaded from a DSpace repository. https://dspace.org/

East African Journal of Swahili Studies
eajss.eanso.org
Volume 4, Issue 1, 2019
ISSN: 1476-4687

EAST AFRICAN NATURE & SCIENCE ORGANIZATION

*Original Article*

# DARASA ZA KIMAHARAJANI ZA NYAKANGA-KUNGWI-SHEIKH JUMA AMIRI KUHUSU UNYUMBA[1]

*Dkt. Mohamed Karama*

Chuo Kikuu cha Kabianga, SLP 2030 – 20200, Kericho, Kenya, mkarama@kabianga.ac.ke.

**Article history:**

*Received: 30 Sep 2019*
*Accepted: 30 Oct 2019*
*Published: 15 Nov 2019*

**Keywords**:

*Usemezano,*
*Unyumba,*
*Maharajani*

## IKISIRI

Lugha ya kimaharajani iliangaziwa mwanzo na Mikhail Bakhtin, mwanaisimu wa Kirusi na mwitifaki mkuu wa Usemezano. Lugha hii ina sifa za kuweka kanro kaida za usemaji wa kirasmi na kuwacha wananchi watangamane bila vizuizi vya kiutawala. Hudhihirisha bezo, ucheshi, upuzi kwa uwazi na kila mshiriki akafurahiya hali hii. Kulingana na Bakhtin niya haswa ni kupata hisiya za nrani za watawaliwa, lakini kwa kauli nyengine, watawala huzitumiya fununu hizi kuzidi kuwatawala wananchi; hichi ndicho kinaya cha umaharajani. Katika lugha na fasihi ya Kiswahili dhana ya umaharajani bado haijashughulikiwa ipasavyo seuze maswala ya kidini. Sheikh Juma Amiri ameweza kupata umaarufu na kuenreleya kualikwa katika hafla mbalimbali Kenya na Afrika Mashariki kwa sababu ya kuelezeya maswala ya unyumba kwa uwazi unaoonesha kukiuka kaida za shekhe wa Kiislamu. Makala haya yameonesha namna Sheikh Juma Amiri anavotumiya maneno, matenro, uigo, sauti, na ishara za mwili kuelezeya mambo ya unyumba namna yalivozorota, yanavozorotesha jumuiya ya Waislamu na anapendekeza mbinu mpya wananrowa wazitumiye ili wafaulishe nrowa zao. Anasuta wanaume, wanawake, mashekhe, wazazi kwa maneno yaliyojaa jazanra na piya hutumiya maneno yatakayochukuliwa ni kufuru lau si umaharajani. Anapomaliza darasa zake hadhira inachanganyikiwa kutojuwa Sheikh Juma Amiri ni nyakanga, kungwi, au ni shekhe? Makala haya yanahitimisha kuwa kwa kutumiya mbinu hii ya kimaharajani, Sheikh Juma Amiri amefaulu kufikisha ujumbe wake kiucheshi na kuwateka kimawazo walengwa watake kumsikiza kila mahali kila wakati.

[1] Namshukuru Ustadh Mahmoud Mau wa Lamu, Mbarak Abdulkadir wa Gede Museum, Malinri, Prof. Issa Mwamzandi wa University of Kabianga, na Khalid Kitito wa Kenya Heritage Training Institute, Mambasa kwa mawazo yao wakati wa mijadala tulokuwa nayo wakati wa utafiti na uandishi wa makala haya.

## UTANGULIZI

Makala haya yanadhihirisha umaharajani uliyomo nrani ya darasa za Sheikh Juma Amiri (SJA) na namna uwasilishaji wake unavofikisha ujumbe wa unyumba kwa hadhira yake. Umaarufu wa SJA umetangaa kote katika Kenya na Afrika Mashariki kwa ulinganiyaji wa dini ya Kiislamu. Ni mmoja wa maimamu wa Msikiti wa Jamia, Nairobi, Kenya. Ana darasa zake anazoenresha kuhusu mafunzo ya dini hiyo katika msikiti huo. Hivi karibuni, umaarufu wake umeongezeka hadi taasisi za kiserikali za Kenya zimemtambuwa kati ya watu maarufu nchini Kenya na walimshirikisha katika kampeni za kueneza amani wakati wa Uchaguzi Mkuu wa 2013. Juu ya umaarufu huu na kutambuliwa huku katika mawanda ya kijamii, hakuna makala yoyote tuliyoyapata, wakati wa utafiti wetu, yaliyoandikwa kumhusu shekhe huyu wala anayoyazungumziya. Makala yetu yanaazimiya kuchangiya katika taalimu kuhusu darasa zake za kimaharajani zilizomleteya umaarufu wa kupendwa na kuzirwa na baadhi ya wasikilizaji wa darasa zake kama hisiya alizokumbana nazo Nafzawi (1886) alipoandika kuhusu mada hii ya unyumba katika mawanda ya Uislamu zama hizo.

### Umaharajani na sifa zake

Kulingana na *The Penguin Dictionary of Literary Terms and Literary Theory* (1999) inaeleza maharajani kuwa, "maharajani asili yake ni sherehe mahususi iliyosherehekewa na Wakatoliki. Ni sherehe kabla ya saumu ya *Lent* kabla ya maadhimisho ya Pasaka. Kwa ujumla, ni sherehe yenye tamasha nyingi za kula na kunwa, furaha na shamrashamra ainati. Muda ulipopita, nrani ya tamasha hizi kukawa na mionroko ya kudhihaki utawala au ngazi za uongozi kutoka kwa wananchi wa kawaida". Mwitifaki mkuu wa Usemezano, Mikhail Bakhtin (1895–1975) nriye aliyekuja kuonesha kuwa matukiyo haya ya kimaharajani yanadhihiri katika mazungumzo ya lugha ya watu wa kawaida.  Umaharajani unaonekana wakati lugha ambazo hazichungi kaida za kisarufi wala "adabu" za kimazungumzo zinapotumiwa baina ya watu wa kawaida na kati yao na waungwana wa mji. Lugha hii ya kikawaida ameiita *skaz* na ile hali ya kuweka kanro miko ya lugha wakati wa tamasha ameiita umaharajani (Holquist, 1981).

Sifa kuu zinazobayanisha umaharajani ni matumizi ya lugha za unenibezi zenye tabiya mbovu, maneno na matenro yasiyopendeza, na kila aina ya kauli chafu zenye kwenda kinyume na miko ya uzungumzaji wa kidasturi (Morris, 199). Piya, kuna matumizi ya taswira za kinyago zenye kuonesha picha isiyoeleweka kutokana na lugha ya kitepetevu inayotumika wakati wa sherehe hiyo. Fauka ya hayo, taswira za kidhifa za makulati zisizo za kawaida hutumiwa ili kudhihaki ulafi wa wanajamii na watawala wao. Hatimaye, kuna matumizi ya taswira za uchi na viungo vinavohusika na uzao wa mwanadamu ili kuweka wazi mambo yanayositiriwa wakati wa maongezi ya kikawaida; hutumika kama jazanda ya ufufuwo unaotokana na viungo hivi va mwanadamu. Taswira hizi zenye kubeba maana pevu kuhusu mawazo ya bezo la wanajamii kudhihaki mionroko ya kijamii huleta afueni katika jamii. Sifa zote hizi zinajitokeza wakati wa tamasha hilo la maharajani linalotawaliwa na kicheko ambacho huwa pana kiupeo na hujumuisha kila mshiriki nrani ya tamasha, na hubeza kiukosowaji matukiyo rasmi katika jamii halisi.

Niya ya umaharajani ni kuchekeleya utawala unaodhihirika kwa kuwako matabaka ya kijamii katika jamii moja. Matabaka haya hutafautisha wanajamii kidini, kimali, kicheo, kijinsiya, kilugha na kila hali ya kijamii; kuna tabaka la juu (waungwana, watawala) na la chini (wajakazi, watawaliwa). Wanatabaka la chini hutumiya nafasi hii ya umaharajani kueleza hisiya zao kwa kuigiza waliyoko kwenye mamlaka na kubeza wanayoyafanya wanatabaka la juu. Matenro haya yote yanatokeya katika wakati wa umaharajani pekee ambapo kaida zote za unenaji zimewekwa kanro, kinyume na asemavo Mwamzandi (2002) kuwa zimeonrolewa, na matabaka yamegeuzwa juu-chini chini-juu. Baada ya maharajani mamlaka na matabaka haya ya kijamii na ya kilugha hurudiya katika hali yake ya mwanzo. Kulingana na Bakhtin, umaharajani ulikuwa na athari chanya kijamii kwani uliwawezesha wanajamii kutowa hisiya zao za nrani kuhusu utawala wa jamii hiyo. Athari kinyume ya umaharajani kwa wajakazi ni ya upanga kupata kuwili. Kulingana na Bernstein (1986:106) anaeleza kwamba kuwawacha wanatabaka kutangamana bila ya vizuwizi va kidasturi kunamfanya mtawala kujuwa yaliyomo katika jamii na piya kudhibiti mashiko yake juu ya

mamlaka yake. Watawala wataenreleya kuvumbuwa mbinu mpya za kujidhibiti mamlakani kwani baada ya maharajani hali inarudi kama ilivokuwa mwanzo.

**Maharajani Uswahilini**

Nilipozungumza na Mbarak Abdulkadir, aliyekuwa mkuu wa makumbusho ya Lamu sasa Gede, Malinri, Kenya alinambiya kwamba zilikuwako ngoma za aina ya kimaharajani Uswahilini. Wakati wa maombolezi ya bi kikongwe katika familiya, wajukuu wake 'walisherehekeya' kifo chake na kuvaa koja la chakula kama mahamri, kaimati, mofa, bajiya kwenye shingo zao na kucheza ngoma. Hata hivyo, alinambiya sherehe hizi zilipigwa marufuku katika 1954 na Chifu wa Faza, Kaunti ya Lamu. Ustadh Mahmoud Abdulqadir wa Lamu, alinieleza piya kuhusu ngoma hii ya kusherehekeya kifo cha bi kikongwe, lakini yeye alinambiya si ya Waswahili bali walokuwa wakiicheza ni watumwa waliyoishi visiwani Lamu. Lodhi & Westerlund (1997) wanasema kuwa umaharajani unaonekana katika sherehe za nairuzi ambazo husherehekewa mnamo Agosti wakati wa mwanzo/mwisho wa mwaka wa Kiswahili. Wengine huiita sherehe hii kuoga mwaka. Krapf (1882) katika kamusi lake ameeleza kuwa sherehe hii ya nairuzi ilikuwako katika utawala wa Sultani Khalifa lakini aliipiga marufuku kwa sababu washerehekeaji walikuwa wakivunja sheria za utawala huku wakisema ni nguzo moja ya sherehe hizo.

Pahala pengine ambapo umaharajani unadhihiri piya ni katika mafunzo ya jandoni na unyagoni: wavulana na wasichana wanapopelekwa sehemu fulani vijijini mwao kupashwa tohara na kupanrishwa daraja ya utuzimani, na kufunzwa maswala ya unyumba. Mafunzo ya unyumba hugusiya maelezo ya kuwa mvuli na havule, uchumba, kuowana, tenro la kujamiiyana, siku na wakati wa kuowana, namna ya kuenresha nyumba mume na mke, kuepukana na fitina za kuvunja nyumba ya bwana na bibi, na namna ya kusuluhisha migogoro ya unyumba inapoibuka. Kadhiya ya jando na unyago inapatikana mwote Uswahilini kama Cory, (1948) alivofafanuwa kwa tafsili.

Maelezo ya Shariff (1991) yanaafiki mawazo yetu kwamba maudhui na fani ya kimaharajani yanapatikana katika fasihi ya Kiswahili tangu zamani hadi sasa. Akilenga zaidi ushairi wa Kiswahili, Shariff anasema kwamba pana ushahidi wa maudhui ainati kuanziya ya kidini, kijamii na kisiasa. Mashairi mengi yaliyohifadhiwa katika maktaba mbalimbali Ulaya na kwengineko yanazungumziya maswala ya kiduniya kuliko kuzungumziya ya kidini. Kuna tenzi na mashairi yanayomzungumziya Mtume Muhammad na mitume wengine na piya kuna mashairi yanayozungumziya mapenzi, maadili ya kijamii, na ungono. Kwa mfano, shairi Utenzi wa Mwanamanga , Shariff (1988:93) anaeleza kuwa halikuanza na kaida ya kutaja Mungu kwanza kwa sababu lilikuwa ni shairi la 'kiasharati' (kingono) lililotungwa na shujaa na manju Fumo Liyongo kumsifiya mkewe. Lugha hii ya kishairi huwa imesheheni jazanra, tashbihi, na mafumbo na huonesha ubingwa wa mtunzi kilugha na piya huonesha 'ustaarabu' wakati wa kuzungumziya maswala nyeti ya kijamii kama ngono. Mwamzandi (ashatajwa) amefaulu kuonesha ainati za kauli chafu na matenro machafu yanayotokeya katika nyimbo na ngoma za taarabu huku Uswahilini yanayoashiriya umaharajani uliyomo kwenye utanzu wa fasihi hiyo. Maoni yetu yanatafautiyana na ya Mwamzandi kwa sababu yeye ametenganisha dini na matenro ya kijamii, kwa mfano nrowa, ilhali, SJA anasema yote, dini na jamii, ni kitu kimoja na havitenganishiki katika muktadha wa Kiislamu. Kwa kuyaelezeya maswala ya unyumba kwa nadhari ya kidini nrimo tunamouwona umaharajani ukijitokeza kwa sababu hadhira iliyoko inashangwazwa na vituko vinavojiri kwenye darasa hizo.

**MBINU ZA KUKUSANYA DATA NA UPEO**

Finnegan (2012) ameangaziya fasihi simulizi katika pembe zote za Afrika. Nranimwe ameeleza kuhusu ulumbi wa waafrika, sifa zao na namna wanavoheshimiwa katika jamii za kiafrika. Kazi yake imetupa mwangaza wa kumulikiya ulumbi alonao SJA katika fani ya unyumba na haswa tukiangaziya darasa zake za kimaharajani. Darasa za SJA zinamfanya aonroke kwenye tabaka la shekhe wa dini lenye miko ya uzungumzaji wa kishekhe na kumfanya awe nyakanga au kungwi katika mafunzo yake ya unyumba.

Tulimtauwa SJA kwa sababu ya upekee wa darasa zake za kimaharajani na yeye mwenyewe

hajashughulikiwa kitaalamu juu ya umaarufu wake Afrika Mashariki. Data yetu ya kimsingi tuliipata kutoka kanra za nyakaninga (NN) zinazopatikana katika tovuti ya youtube.com. SJA amezungumziya maudhui kadha wa kadha kuhusu dini ya Kiislamu lakini utafiti wetu ulijikita katika darasa zake za unyumba. Tulitauwa kanra kumi zenye mada za unyumba pekee ijapokuwa katika mtanrao huwo kunazo nyakaninga nyengine zake kuhusu mada nyengine. Uchanganuzi wetu ulishughulika na data inayohusu matumizi ya kauli ‘chafu’ na jazanra zote kuhusu unyumba, matumizi ya ishara za mwili, viimbo va sauti yake, matenro juu ya jukwaa wakati wa darasa hizo, na maswali ya kibalagha kama alivopendekeza Ali (2013). Mbinu anazotumiya wakati wa uwasilishaji wa darasa zake kutoka maneno anayo(vo)yatumiya, matenro anayoyafanya jukwaani au mimbarini, na sauti anazoziiga na ukiukaji wa urasmi wa uwasilishaji wa kishekhe wa Kiislamu nriyo madhumuni yetu yaliyopambanuwa umaharajani uliyomo nrani ya darasa hizo. Makala haya yamedhihirisha umaharajani uliyomo nrani ya darasa hizi za SJA na hayatoshughulika na kuangliya sababu za umaarufu wake wala kupima umaarufu na athari za darasa hizi kitakwimu. Utaratibu wa uwasilishaji wa uchanganuzi wetu wa data ni wa kimaelezo.

Katika makala haya darasa ina maana ya kikao cha masomo anachokienresha SJA katika kumbi za kijamii na misikitini. Hali kadhalika, kauli chafu ina maana ya maneno/matenro/sauti ambayo hayana tasifida wakati wa kusemwa kwake na piya yanakiuka kaida za usemaji wa kirasmi wa shekhe wa dini ya Kiislamu. Mwamzandi (ashatajwa) aliuita umaharajani ‘shani’ lakini sisi hatuwafiki istilahi hiyo kutokana na ukuruba wake na maana ya ‘miujiza’, kwetu sisi umaharajani limewafiki kuwa ni hali ya kuwekwa kanro adabu za unenaji katika mazungumzo ya unyumba. Unenibezi umetumika kwa maana ya lugha ya shere ya kuchekelea na kudharau jambo linalofanyika katika jamii kwa minajili ya kulikosowa. Dhihaka au mzaha ina maana ya kuchekeleya jambo lakini kwa niya ya kufurahisha zaidi kuliko kukosowa. Unyumba unamaanisha hali baada ya fungamano la kuowana baina mume na mke. Unyumba unajumuisha maswala yote ya kinrowa kutoka kujamiiyana, kubembelezana, kuchukuliyana kitabiya, kutekelezeyana haki za kiusimamizi nrani ya nyumba mpaka kushika mimba, umito, na mazazi; yote ni unyumba kijamii na wala haifungamani na sheriya za dini. Kuhusu masomo ya unyumba katika mila za Uswahilini, kuna nyakanga ambaye ni mwalimu mwanamume anayewafunza mabarobaro katika jando na kungwi ambaye ni mwalimu mwanamke wa wasichana katika unyago na tumeafiki kama walivoeleza Cory (1947) na Fair (1996) mtawaliya. Kuhusu maswala ya kidini tumetumiya shekhe kwa maana ya mwalimu wa dini.

## MIONROKO YA SHEKHE KATIKA MAFUNZO

Masomo ya dini ya Kiislamu yanachukuwa uregelezi wake kutoka kitabu kitakatifu cha *Kuruani*. Nranimwe mumeelezwa maswala mbalimbali kuhusu imani na matenro yanayomkurubisha mja kumjuwa na kumuabudu Allah. Elimu hii ya imani na matenro imetiliwa sherehe na Mtume Muhammad ambaye ametumilizwa ili kuwafahamisha waumini kuhusu Allah. Panapotokeya jambo ambalo lahitaji ufafanuzi na halipatikani katika kitabu hicho au maneno ya Mtume, basi huangaliwa kauli ya pamoja ya wanazuwoni kuhusu jambo hilo na ikishinrikana basi mwanachuwoni wa kuaminika hutumiya kipimo cha hekima alonayo kufutu kuhusu suala lililoko mbele yake na suala kama hilo katika maelezo ya waliyotanguliya kiusomi. Hizi nrizo nyusuli za ufahamu katika Uislamu (Draz, 2008).

Ghazali (1993) alipokuwa akielezeya aina za elimu katika Uislamu alisema kuna elimu za lazima (za imani na matenro yanayowajibikiwa), elimu ya makuruhu kutokana na kushabihiana kwake na uharamu, piya ameeleza kuna na elimu ya kusaidiya jamii ili ipate kutengeneya na kuenreleya. Katika elimu hii ya kutosheleza jamii ametaja fani kama za ukulima, usimamizi, ufundi, ushonaji na piya elimu kama ushairi, mapisi, jiografiya, na bayolojiya kwamba ni elimu za kukubalika katika Uislamu. Kwetu sisi elimu anayoisomesha SJA inajumuika katika aina hii ya tatu. Hali kadhalika, Ghazali ameeleza na kumtukuza mwalimu kwa daraja alizozitaja Mungu na Mtume wake. Halafu anaregeleya aya ya *Kuruani* (16:125) inayosema, “linganiya [funza] katika njiya ya Mola wako kwa hikima na mawaidha mema” na kushadidiya hoja ya kuwa mwanachuwoni, kwa maneno ya Mtume

Muhammad, kwamba akimsomesha mtu mmoja na Mungu Akamuongowa kwa sababu yako ni bora kuliko ardhi yote na vilivomo. Ghazali (ashatajwa) akakokoteza tena kwamba Mtume Muhammad amesema kuwa elimu ipatwe kwa sababu kuipata ni kumcha Mungu, kuitafiti ni ibada, kuitalii ni jihadi, kuifunza kwa mtu asiyejuwa ni zaka (sadaka), na kuwapa wanaostahiki ni taadhima. Kwa minatarafu ya maelezo haya, tunakubaliyana kwamba masomo anayoyafanya SJA yamechimbuka katika nasi ya *Kuruani* na mwenenro wa Mtume Muhammad.

Ghazali (1993) na Abulquasem (1979) wamezungumziya kuhusu elimu – faida, sifa, dalili za mwanachuwoni bora – piya wameelezeya kuhusu mahusiyano ya mwalimu na wanafunzi wake. Wameyaainisha mahusiyano hayo kwa kuyaita majukumu yake juu ya wanafunzi na kuyaritibisha hivi: Aoneshe huruma na kite kwa wanafunzi wake kama watoto wake; afwate mwenenro wa Mtume Muhammad kwa ukamilifu; asifiche au kuhini mashauri yoyote kwa wanafunzi wake; awakataze kufanya maasiya kwa njiya nzuri na tahadhari sana; asidharau mwalimu au elimu nyingine mbele ya wanafunzi; awafunze kwa kiwango cha welewa wao; awafunze kwa daraja moja moja siyo kufululiza; *asifanye mzaha au kucheka nao* (msisitizo wetu); na yeye mwalimu afanye matenro yanayolingana na maneno yake.

Tukichukuwa dalili nyengine kutoka kwa matenro ya Mwalimu wa Mashekhe wa Kiislamu, Mtume Muhammad, tunauwona ukali wake unavojitokeza wakati anapozungumziya maswala ya kutuna katika Uislamu. Mtume Muhammad alipokuwa akielezeya maswahaba zake kuhusu wasiya juu ya wanawake wao (mabibi zao) maswahaba walicheka aliposema kwamba mume anampiga mkewe kipigo cha kinyama halafu anatarajiya usiku ule ule alale naye atake kustarehe naye. Mtume alikuja juu kwa hasira alipowaona wanacheka kwa sababu ni jambo wanalifanya maswahaba. Kauli nyengine inasema mmoja kati ya maswahaba alitokwa na upepo nriyo wakacheka. Lakini katika fasiri ya hadithi hiyo Shekh Nassor Bachu (2013) anasema kwamba Imam Nawawi (h.t: 95) katika maelezo yake kuhusu Hadith Na. 274 maswahaba walicheka kutokana na kitenro hicho cha mmoja wao kutowa upepo, na inaweza kuwa piya, ni kwa sababu ya tabiya ya kupiga wake waliyokuwa nayo nriyo wakafanyiyana mzaha mbele yake na likamuudhi Mtume Muhammad. Shekh Nassor Bachu anaenreleya kusema kuwa Mtume anapowahutubiya waislamu macho yake huwa mekunru kutokana na utunaji wa mada ya kuwadhulumu wanawake na wakalifanya liwe ni la mzaha au kuchekesha. Kutokana na maelezo haya ya hadithi hiyo ya unyumba tunaona hakuna mzaha wala kucheka mbele ya mwalimu. Tumehitari kuchukuwa moja kwa moja kutoka masomi ya walimu wa dini ya Kiislamu kwa sababu lengo letu la utafiti limo katika kudhihirisha kinyume cha yanayosomeshwa katika dini na anayoyafanya SJA wakati wa kufikiliza ujumbe wake, ambalo nrilo lengo la umaharajani – hali ya kinyume-mbele-juu-chini-chini-juu.

## DARASA ZA SJA KUHUSU UNYUMBA

Kama tulivokwishataja hapo awali kuwa SJA ni shekhe na imamu wa msikiti. Ni mzawa wa Takaungu, Kaunti ya Kilifi (amelitaja katika NN 2b & 6b) na anazungumza darasa zake kwa Kimvita na hutaja aya za *Kuruani* na maneno ya Mtume Muhammad kwa Kiarabu na huzifasiri kwa Kiswahili. Amezungumziya mada mbalimbali kuhusu Uislamu lakini mada ambayo imemleteya umaarufu zaidi ni darasa za unyumba. Hili linadhihirika katika idadi ya utizamaji (wa waislamu na wasiyokuwa waislamu [maneno ya watizamaji katika NN 2b]) ambao umefikiya malaki kwa idadi za wapendaji na wasopenda wa kanra zake za unyumba katika youtube.com. Kwa mfano, NN 1b, NN 2 (imepita laki mbili), NN 2b, NN 5 ambazo zimepita laki moja na nusu na zaenreleya kutizamwa. Kinyume na kanra zake ambazo hazizungumzii mada hii ya unyumba, kwa mfano, NN 5b yenye kuzungumziya miujiza ya Allah imetizamwa mara elfu ishirini na mbili mpaka tulipokuwa twaandika makala haya. Kulingana na maelezo yake amealikwa kwingi katika Afrika Mashariki kuzungumziya mada hii ya unyumba na wengi wamemhakikishiya kufaidika kwao kutokana na darasa hizi.

Darasa za SJA kuhusu unyumba zina maelezo ya mambo yanayofanyika nrani ya tangamano la nrowa kutoka mandhari ya ofisini, nyumbani, sabuleni, jikoni, chumbani mwa wenye nyumba mpaka wanayoyafanya kitanrani. Huanza kwa kudonrowa aya za *Kuruani* na maneno ya Mtume Muhammad kuhusu unyumba na halafu hueleza

waliyoyasema mashekhe wa dini kuhusu mambo haya. Hata hivo, sehemu kubwa ya darasa zake ni sherehe na maelezo ya kina anayoyatowa ili kutiliya mkazo au kuthibitisha yaliyosemwa na *Kuruani* na Mtume Muhammad. Katika maelezo yake huwa hafichi kitu kwa kuzungumza kitasifida kinyume cha *Kuruani* na Mtume Muhammad ambayo hutumiya lugha ya kijazanra na kitasifida, kwa mfano, suala la kumuingiliya mke kwa mbinu gani. Nrani ya darasa hizi hueleza juu ya mambo kadha wa kadha: Sifa za mwanamke au mwanamume mzuri na bora; haki za kila mmoja katika nyumba kumtenreya mwenziwe; njiya za kuzifanya nrowa zifaulu; maneno ya kimapenzi yanayofaa kuambizana baina ya wananrowa; namna ya kuchukuliyana kitabiya; na piya namna ya kutoshelezana kingono.

Niya yake ya kuzungumziya mambo haya ya unyumba yametokana na masomo haya kuepukwa kufunzwa wananrowa wanapotaka kuowana (NN 1b & NN 4). Kulingana na yeye wananrowa wanaingiya katika marahala mapya ya unyumba bila ya fununu ya majukumu wanayotakikana kufanyiyana ili nrowa idumu. Sikitiko lake ni kwamba maswala haya yamewachiwa mashule ya kirasmi na mafunzo ya kimila; mashekhe wa dini ya Kiislamu wameyapuuza kwa kutokuyaelezeya waumini. Katika mafafanuzi yake anaonesha kwamba mionroko ya dini ya Kiislamu yanaingiya katika maisha yote ya muumini na kwamba mada zote lazima zifunzwe na zieleweshwe ili jamii nzima itengenee (NN 4). Kutengeneya huku kutatokana na kuyasomesha mambo haya kwa uwazi unaotakikana na wala siyo kustaajabiya kwamba ni upuzi au matusi na watu kupiga ‘Lahaula!’ nyingi kwamba hayafai kusemwa hadharani (NN 3b).

Darasa hizi zimeleta hisiya mchanganyiko miongoni mwa waumini waislamu. Kuna waumini wanaompongeza kwa kuyaeleza yasiyoelezeka hadharani kwenye kumbi za wanajamii na hata kwenye mimbari msikitini, kulingana na maoni yetu hawa ni wengi. Kuna na waumini ambao wamepinga mada hizi kuletwa hadharani haswa msikitini na mbele za umati wa watu. Kuna na wanaopinga mbinu za kimaharajani kama matumizi ya unenibezi, dhihaka, na uigizaji kwenye jukwaa anazotumiya SJA ambazo wanaziona ni kinyume na matarajiyo ya ustahiki wa shekhe wa Kiislamu.

## UMAHARAJANI KATIKA DARASA ZA SJA

Katika sehemu zilizotanguliya tumeeleza maana ya umaharajani na sifa zake. Piya tumefafanuwa mionroko ya mashekhe juu ya wanafunzi wao. Katika sehemu hii tunataka kubayanisha umaharajani unavojitokeza katika darasa za SJA kwa mintarafu ya maneno anayoyatumiya na matenro anayoyafanya jukwaani, katika kumbi za kijamii na juu ya mimbari msikitini, wakati wa darasa za unyumba. Tutaangaziya kauli za mandhari ya kinyago na/au kijanro, lugha ya sokoni, matenro anayoyafanya jukwaani, uigizaji anaoufanya, matumizi ya ishara za mwili, na muda mzima wa mchezo jukwaani pamoja na uhalisiya baada ya darasa.

### Mandhari ya kinyago/kijanro:

Finnegan (2012) anaeleza kuwa mandhari yana jukumu kubwa katika kufaulisha ujumbe wa mlumbi katika fasihi simulizi, hivo basi, nrilo jambo linalofanywa kwanza baada ya jukwaa kutengenezwa; linapambwa kuwafiki maudhui ya darasa. Cory (1947) anatwambiya kuwa wakati mabarobaro wa Kiswahili walipotaka kupashwa tohara walijengewa makazi maalumu nje ya kikowa cha kijiji yanayoitwa Kumbi. Humo janroni nrimo shughuli yote ya tohara na mafunzo ya utuzima hufanywa kwa mabarobaro hao. Fair (1996) anatwambiya katika Zanzibar wanawake wa familiya za kifalme walinunuliwa jumba mahasusi na Sultani kwa ajili ya shughuli ya unyago ambamo mahavule (wa kisultani na kimiji) walikwenra kufunzwa mambo ya kiutuzima. Sawiya katika darasa za SJA jambo hili la mahali mahasusi piya linapatikana. Darasa huzienresha kwa kualikwa katika kumbi za mijini (NN 1b), msikitini (NN 2b), au hata katika madrasa za mitaani (NN 6b). Shariff (1991) anasema kuwa misikiti na madrasa nriyo mahali pa mafunzo yote ya dini ya Kiislamu. Imebayanika wazi kwamba kuna mahali maalumu pa kuenresheya darasa hizi sawa na kama utamaduni unavofanya kuhusu masomi ya unyumba.

Hadhira yake si ya kiutenganishi kama janroni na unyagoni bali inaweza kuwa wanawake/wanaume watupu au mkusanyiko wa wanawake na wanaume pamoja, au, hata mabarobaro ambao bado hawajafikiya makamo ya utuzima nao piya ni

miongoni mwa hadhira (NN 3b). Katika janro na unyago palikuwa na sheriya kali na wasohusika hawakubaliwi kukaribiya hapo. Maneno na matenro yanayofanywa humo ni ya unyumba na huhusisha matusi yanayosemwa hapo tu na wala hayatolewi nje. Kuna walimu wa janroni wanaoitwa nyakanga na wa unyagoni wanaoitwa kungwi. SJA katika darasa hizi anachukuwa jukumu la walimu watatu – ni nyakanga, ni kungwi, na ni shekhe wa dini. Anayatowa maneno haya ya siri kwa uwazi katika hadhara anazoalikwa, kwa mfano, anapozungumziya matiti ya wasichana yalivosimama (NN 4), 'kugusagusa' (NN 4) '*application*' kwa maana ya ngono (NN 3b), shosho kumwangaliya msichana ni bikira (NN 4), na kutaja sidiriya katika msikiti mbele ya wanaume watupu (NN 2b) na darasa hizi hupeperushwa hewani kwenye kanra za nyakaninga mitanraoni kwa kila mtu kufaidika kwazo.

Kama ilivo kwamba maharajani ni tamasha la mahali, wakati, na lengo maalumu katika jamii za ulimwenguni, vilevile, darasa za SJA tunazikuta zikifanywa katika mahala na mada maalumu lakini nyakati tafauti tafauti katika takwimu ya hadhira. Wakati wa maharajani za kijamii washiriki wote hutangamana bila mipangiliyo maalumu ya kiutenganishi wala hapana sheriya za kaida ya mambo. Katika darasa za SJA, ijapokuwa kuna kukutana kwa jinsiya zote mbili au tafauti katika mahala pamoja, utangamano unapatikana kwa kuelezwa mada moja jinsiya zote mbili na shekhe ambaye amevuwa jukumu la ushekhe na uwalii wa dini na kuvaa vazi la nyakanga na kungwi pamoja, sawiya akiwa ukumbi wa kijamii au msikitini. Hili la kuchanganya majukumu yote matatu (unyakanga, ukungwi, ushekhe, au 'mzee' (NN 4)) kwa pamoja nriyo tasnifu ya SJA kwamba dini ni kila kitu katika maisha ya mwanadamu na kwamba hata Mtume Muhammad alikuwa hivo. Kwa kuwekwa kanro tafauti za kijinsiya katika mandhari na mada moja ya darasa hizi nripo umaharajani unapodhihirika.

## Lugha na umaharajani

Lugha nricho chombo atumiyacho binadamu ili kufikisha ujumbe anaotaka kuwasilisha. Kuna vipashiyo kadhaa anavovitumiya katika ujumbe huwo kama foni, fonimu, mofimu, leksimu, sentensi, kauli ambavo vikikutanishwa katika mtongoo huleta maana katika ujumbe. Holquist (1981) anasema kwamba vipashiyo hivi tukivijumuisha pamoja na: niya ya msemaji, usuli wa neno, mapisi yake, muktadha vilimotumika, viziada sauti, ishara za mwili, lahaja, na sajili maana haswa itajulikana na mawasiliyano yatakamilika. Hivo basi, Bakhtin anasisitiza kwamba kujuwa maana ni kutafiti lugha ya maudhui pamoja na mitinro ya uwasilishaji katika kauli nzima kimchanganyiko bila kufarikisha mojawapo. Katika sehemu hii tutaangaziya data ya matumizi ya lugha namna SJA anavoitumiya kuwasilisha ujumbe wake.

### *Lugha ya sokoni*

Matumizi ya lugha ya sokoni ni moja kati ya sifa za umaharajani zinazojitokeza katika tamasha na hujulikana kwa matumizi ya lugha ambayo ni huru, wazi, na ya kuchekesha. Kulingana na Holquist (1981) katika mawanda haya ya maharajani hakuna kaida wala tasifida katika matumizi ya lugha. Maneno kama maapizo, kufuru, matusi ya mtu au uchi wake, hupata maana mpya katika muktadha huu na huleta hali ya kuchukuliyana, uwazi, uhuru, na mtizamo mpya wa ulimwengu huu mpya. Ameiita lugha ya kisokoni kwa sababu ni sokoni ambapo kuna mkusanyiko wa aina zote za lugha ambazo huenra kinyume na kaida za kisarufi na kisemantiki katika hali ya kirasmi. Katika hali hii ya kubobojekwa na maneno machafu, dhihaka na mizaha, muuzaji hatukani bali anawachekesha wanunuzi ili waje wanunuwe bidhaa zake.

### *Maneno ya matusi*

SJA anatumiya lahaja ya Kimvita katika darasa zake zote na piya huchanganya na 'sheng' (NN 6b & 2b) kwa sababu ya kukaa sana bara (Nairobi) na Pwani sasa amekuwa 'mkimbizi' (NN 6b). Katika data yetu kuna matumizi ya maneno machafu kama 'upuzi', 'upumbavu', 'ujinga' (NN 5), 'ufala', 'uzutwe', 'ushamba' (NN 2b) kuwaelezeya mume na mke wasiyojuwa namna ya kuishi kinyumba. Ametumiya neno 'negro' kwa maana ya mwanamume wa miraba minne (NN 6b). Neno 'negro' ni tusi lililotumiwa na Waamerika weupe kuwaita Waafrika lakini Pwani ya Kenya lilimaanisha mtu mweusi mwenye umbo kubwa. Neno 'mwanaharamu' (NN 4), Mtume Muhammad ni kizee cha 'kishihiri' (NN 2b) yenye maana ya

mtu mjanja na kizee cha Kiarabu mtawaliya ni maneno yanayotumiwa mitaani Pwani ya Kenya na wenye kuambiwa maneno hayo hukasirika kutumiliwa maneno hayo.

Data yetu ilidhihirisha kupatikana maneno yenye hisiya za kingono ijapokuwa aliyataja kwa Kiingereza kama: *apple* (kumaanisha matiti), *romantic*, *lips*, *hot kisses*, *hugging* (NN 4), *I love you*, *handsome* (NN 2). Fungu la maneno ya awali aliyatumiya wakati alipokuwa akimueleza Mtume Muhammad namna alivokuwa akiamiliyana na wakeze nyumbani kwake. Piya pana matumizi ya msemo aliyouunra yeye 'maziwa ya mtu anwe mtu, maziwa ya ng'ombe anwe ng'ombe' (NN 5) wakati alipokuwa akielezeya kuhusu mama kunyonyesha watoto wake bila ya kufikiriya sana umbile la matiti yake baadaye. Kunadhihiri katika data tuliyokusanya matumizi ya chuku nyingi katika maelezo yake. Kwa mfano, Bibi anapokwenra harusini anaona aina za mitanriyo mia mbili (NN 5) kuonesha kutotosheka kwa mke juu ya alichonacho yeye na kutaka kama vya wanawake wengine.

### *Vidahizo kama ithibati*

SJA amejaribu katika maelezo yake kujikita katika kutowa hoja na kuidhibiti kwa kutaja maneno ya *Kuruani* au Mtume Muhammad. Tadmini hii inadhihiri katika matumizi ya hadithi hiyo hiyo ya Mtume Muhammad, 'mbora wenu ni yule aliyebora kwa watu wake wa nyumbani (mkewe)' (NN 6b). Hii ni sifa ya maneno ya kimtaani ambapo maneno yanaregelewa ili kusisitiza au kuonesha kwamba hana mengine. Wakati wa kueleza maelezo ya Mtume alitaja maswala ya posa zilizoletwa za bibi mmoja kuwa 2 katika (NN 1b) na 3 katika (NN 6b). Kwetu sisi hii ni ithibati ya kutumiya mbinu za kingano za fasihi simulizi ambapo msimulizi huweza kutafautiyana katika maelezo yake na ikawa hajafanya makosa kifasihi bali ni upotoshaji kitaalamu.

Data yetu imedhihirisha matumizi ya vidahizo kama njiya muwafaka ya kuthibitisha anayoyasema SJA. Anatumiya maelezo ya tajiriba zake nyumbani kwake na maishani mwake na mashitaka anayoletewa ofisini mwake kuhusu unyumba au kutowa mawazo kutoka vipinri va runinga kuhusu jamii kama 'Tyra' (NN 5) na kuwashangaza hadhira yake kwamba huangaliya vipinri hivi (NN 1b) badala ya ushahidi wa kitabuni kama ithibati ya anayozungumziya. Mara nyengine husoma kitabuni lakini sherehe ya aliyosoma nriyo yanayoonesha umaharajani. Kimawazo yake haoni ubaya wowote kupata maarifa kutoka chimbo za kiteknolojiya ya kisasa kwani anakubali wananrowa/wanawake waangaliye vipinri va runinga, kwa tahadhari, kama *blue movie*, sinema za ngono (NN 4) vinavopigiwa kelele na mashekhe wengine (NN 5). SJA anawapa wanawake hamasa ya kusimamiya nyumba zao (NN 6b & 2b) na kuzidhibiti nripo watakapowaweza waume zao na kuwatiya katika himaya yao. Haya anayafanya bila ya kuwatoleya aya wala maneno ya Mtume bali ni naswaha yake ya 'kizee'.

### *Kutweza cheo*

Darasa za SJA zimedhihirisha utwezaji wa vyeo va wanaume wenye ubabe, wanawake wavivu, vijana wasojuwa unyumba na walimu wa skuli ambao hawana moja wajuwalo kuhusu elimu hii ya unyumba. Katika kuwatweza huku nriko alikokusisitiziya kwamba waliyoko juu wateremshwe chini na waliyoko chini nao waerevushwe wapanre juu kwenye mamlaka ya nyumba. Anasema hivi kuhusu wanaume mibabe wenye kudhalilisha wanawake akiwaita 'bosi, shekhe, imamu, sultani, haini, na mgandamizaji na kwamba sifa za mume zitajulikana kutokana na mke wake anavomtaja mbele za watu (NN 2b). Wanaoowa bila ya kujuwa sababu ya kuowa hawo ni wajinga wa mwanzo kwa sababu wamedanganyika na uzuri wa sura na maneno matamu ambayo hayajengi nyumba bali ni wingu la kupita maana uzuri hauchelewi kuonroka punre akisha zaa (NN 1b). Au, anaposema "kata puwa yako iwe kiteweo" kwa kuutweza uzuri wa mwanamke kuwa nriyo sababu ya kuolewa. Anazidisha, ikiwa mume ni mjinga huwa 'amekufa' na mwanamke mvivu piya 'amekufa' (NN 5) wote hawo hawawezi kuenresha nyumba. Kimajukumu ya unyumba mke na mume ni sawa hakuna aliyemzidi mwenzake kwa sababu wote lazima wacheze sehemu zao kiukamilifu ili nyumba istakiri. Lalamiko la SJA kuhusu sababu ya kusambaratika nrowa za kisiku hizi ni wazee walipowacha kuwafunza watoto wao masomo ya unyumba na kuwawacha walimu wa maskuli ambao hawana elimu ya dini kuwafunza unyumba

wa Kiislamu (NN 4) ambapo kwa maoni yake ni kinyume cha waziwazi.

### *Maneno ya kufuru*

SJA ni shekhe anayeaminiwa mpaka kupawa uimamu wa msikiti mkubwa Nairobi na kwamba welewa wake wa dini ya Kiislamu ni mpevu mno wa kuweza kutambuwa lipi la sawa lipi la makosa na hapo kuwafunza na wengine. Uwelewa huu wa kidini unaweza kutiliwa shaka kwa matumizi ya maneno ambayo yana taswira ya kukufuru dini ya Kiislamu. Kwa sababu ya muktadha wa maharajani maneno haya yanaeleweka kwamba si kufuru bali ni kughasika kwake na watu kuelewa kimakosa maana ya dini na majumba kuvunjika au kuvurugika kwa sababu hiyo. Data yetu inaonesha matumizi ya 'Lahaula!' (kumuomba Mungu) yaani kustaajabiya anayoyaeleza hadharani kwamba shida za majumbani hazitatuki kwa neno hilo bali ni kuyasema ili watu wafunzike warakibishe hali zao (NN 6b). *Kuruani* imempa fadhila zaidi mwanamume juu ya mwanamke lakini SJA amewateremsha hadhi wanaume wa Kiislamu kuwa wanawake nriyo wanaosema mume yuko vipi nyumbani na hivo mwanamke nriye bora katika unyumba (NN 2b). Data yetu imedhihirsha matumizi ya msemo unaotumiya kitabu kitakatifu cha Waislamu *Kuruani* na piya huitwa msahafu SJA analitaja neno hilo kwa kuonesha bezo na ghasi kwamba, 'misahafu msikitini, nyumbani, chumbani, kitandani (NN 2b). Piya matumizi ya msemo mwengine, 'Tasbihi tuu!, Msahafu tuu!, Kumswaliya Mtume tuu! (NN4) yana malengo hayo hayo ya kubeza. SJA anaonesha kukejeli kwake tabiya ya wanaume na wanawake wanaoshughulika zaidi na dini na wakasahau kwamba penzi lao la kimwili wa kibinadmu piya linahitaji kuangaliwa. Kwa kusema hivi, SJA anamuonesha Mtume Muhammad kuwa mwanamume aliyewajibika nyumbani kwake na kwa wakeze na kuwapa mahitaji yao yote bila kujiona yeye ni bora kuliko mkewe. Taswira hii ya Mtume inamfanya SJA kukiteremsha cheo cha Mtume Muhammad kutoka utume na kumfanya mume wa nyumba yake (NN 2b). Kumleta Mtume katika ubinadamu wake nriyo SJA anapoonesha ithibati ya mafunzo yake kwamba hakiuki sheriya wala mafunzo ya dini lakini lau si muktadha huu wa umaharajani SJA angeeleweka vibaya na kuambiwa ni kufuru afanyayo.

### *Taswira za viungo va uzazi*

Tumesema hapo awali kuwa katika maharajani kuna matumizi wa taswira za viungo vinavopatikana katika sehemu ya chini ya mwili wa binadamu venye kuhusika na uvyazi. Viungo hivi kijazanra huashiriya ufufuwo wa kuzaliwa upya binadamu kutokana navo. Kwa hivo, kuvitaja ni kumshajiisha binadamu avitambuwe umuhimu wake na hana haja ya kuviogopa kuvitaja kwa uwazi. Katika data yetu tumepata matumizi ya jazanra hizi kwengine zimetajwa kwa uwazi kama 'matiti yaliyosimama' au (ma)*apple* (NN 4), au kijazanra kwa mfano umbo la mwanamke kama '*figure* 8 au kama chupa ya *cocacola*' (NN 2 & 6b) kuonesha uzuri wake, au piya '*mic* na shikiyo' (NN 4) kuelezeya vifaa va kujamiyana mke na mume. Wakati SJA anapozitaja sehemu hizi huwataka radhi wasikizaji wake na kuwaambiya hakuna njiya nyengine ya kuwaeleza kuhusu sehemu hizi ila kuzitaja wazi. Kutajwa sehemu hizi kwa njiya ya jazanra pevu (Mwamzandi, ashatajwa) ni kuonesha ubingwa wa matumizi ya lugha ya kitamathali lakini kwetu sisi ni umaharajani kwa shekhe kuzitaja mimbarini au mbele za watu bila kuficha.

### *Matenro*

Kabira (1983) anapoelezeya kuhusu usanii wa watambaji hadithi au walumbi katika jamii za Kiafrika anaonesha kwamba ujumbe utawafikiya wanajamii kutokana na ubingwa wa mtambaji kutumiya maneno pamoja na matenro. Matumizi ya maneno, mabadiliko ya sauti yake, tanakali anazoiga na matumizi ya ishara za mwili husaidiya kuhuisha masimulizi na kuyafanya yawe na kivutiyo na matamu zaidi. Katika data yetu haya yanajitokeza wakati SJA anapotumiya taharuki katika kuelezeya ploti ya tukiyo alilokumbana nalo au anapolisoma kitabuni (NN 1b). Wakati mwengine huivuta nadhari ya hadhira kwa kuwaambiya 'sikilizeni vizuri' au huwaambiya, '*are you ready?*' (NN 2). Piya anatumiya maswali ya balagha (NN 5 & 6b) na kuishirikisha hadhira ili ithibitishe anayoyasema kuhusu tabiya fulani za waume na wake kwa kuwauliza, "ni kweli si kweli?" (NN 6b). Mbali ya kusema hata hutumiya kimya cha sekunre kadhaa katika darasa zake ili hoja aliyoitowa imizike katika mabongo ya hadhira yake (NN 5). SJA hufanya drama jukwaani kwa kuigiza haswa namna mambo yanavotokeya

majumbani (NN 1b). Kwa mfano, namna Mtume Muhammad anavoingiya nyumbani kwake na namna anavonyatiya, kwa adabu, kikao cha mkewe Bibi Aisha na wanawake wengine.

### *Kuigiza unenaji*

Bingwa wa msimuliyaji hadithi katika jamii za Kiafrika ana uwezo piya wa kuiga sauti za wanyama, binadamu ili kutiya ladha maongezi yake na kuivuta hadhira ienrelee kumsikiza. Data yetu imedhihirisha uigizaji wa sauti za vijana wa mitaani, sauti za wanawake (NN 2), sauti za wanaume waarabu (NN 2b) bali piya huigiza tabiya mbaya za wanaume za kuvuta koromo wakati wakiwa wamelala (NN 6b). Uigizaji anakufanya kiuyakinifu mpaka hadhira inafurahikiya uigizaji huu. Mfano anapomuigiza mwanamke ambaye anasingiziya kichwa chamuuma na mwili wote wamtonesha (NN 2). Hata sauti yenyewe anailegeza kumuiga mwanamke huyo. Mfano mwengine ni wakati anapomuiga kijana anayeghasika na umito wa mkewe kwa sababu ya ujauzito wake na kumwambiya afadhali aenre kwao akakamilishe umito na mazazi huko (NN 2).

### *Matumizi ya ishara za mwili*

Kabira (ashatajwa) amejumuisha matenro ya msanii wa kimasimulizi pamoja na matumizi ya ishara za mwili kama ala zinazofaulisha ujumbe wa masimulizi hayo. Data yetu imeonesha kuwako na matumizi ya ishara za mwili. SJA anatumiya ishara hizi akiwa katika kumbi za kijamii na piya kwenye mimbari msikitini. Kwa mfano, anapomuigiza mwanamke kichwa chamuuma mbali ya kuigiza sauti lakini piya anaweka vidole va shahada na gumba kwenye paji la uso na vidole vengine vinaning'iniya kuiga wanawake wanavofanya wanaposhitakiya maumivu (NN 2). Piya anapoigiza namna Mtume Muhammad alivokuwa akiwakumbatiya wakeze na kuwabusu anapoingiya nyumbani na anaonesha kumbatiyo hilo kwa ishara ya mikono kushika kifuwa na mabega yake. Katika kuonesha mamlaka ya wanaume mibabe na wanavofanya nyumbani anaonesha wanavoyakodowa macho yao na shingo inavozungushwa kuonesha ukali walonao wanaume hao (NN 2b). Au, anapoonesha mastaajabu ya mume-shekhe anapoonekana na wenzake kapakatwa na mkewe.

### **Muda wa maharajani na uhalisiya baadaye**

Holquist (1981) anasema kuwa maharajani ina muda wa kufanyika na muda huwo unapokwisha basi hali ya maharajani hugeuka na kuwa tafauti. Sheriya na kaida zote hurudiya palepale na wahusika wa maharajani huchunga heshima zao. Data yetu imeonesha kuwa wakati wa darasa hizo ukiisha na sehemu ya maswali kutoka kwa waliyohudhuriya ikianza, mandhari yanabadilika na kuchukuwa mkonro wa kikao cha kutuna. Vichekesho huisha na majibu ni ya kisheriya kutoka *Kuruani* na maneno ya Mtume Muhammad. Jawabu huwa fupi na maelezo hayana uwelezaji mrefu kama anavofanya wakati wa kikao cha darasa yenyewe (NN 5). Tuligunruwa kuwa utizamaji wa kanra ya maswali na majibu ya darasa hizo (NN 5) ni mchache ikilinganishwa na utizamaji wa kikao chenyewe. Lile nyago la maharajani lililokuwa na uchekeshaji na mizaha mingi wakati wa darasa, analivuwa na kuwa shekhe wa Kiislamu mwenye sura tafauti. Katika hali hii nripo inapodhihiri ile sifa ya kimaharajani ambapo sura ya uhalisiya huu haijulikani kwa sababu nrani na nje ya maharajani hali ya mambo ni tafauti.

## MAFAFANUZI KUHUSU UCHANGANUZI

Shariff katika Mwamzandi (2002) anaeleza kuwa Waswahili wanauzowefu wa kutumiya jazanra pevu katika mazungumzo yao ili kuficha wanayoyasema bila kutasuwa waziwazi kwa kutumiya tasifida wanapotaka kukejeli jambo. Katika kanra zote hakuna hata mahali pamoja ambapo SJA ametowa neno lenyewe haswa la kumtukana mtu au uchi wake waziwazi. Kote ametumiya tamathali za usemi za tasifida na jazanra ili kusema maneno mwiko. Maneno ambayo ni ya kawaida lakini yalipotumika katika muktadha wa kimaharajani yalipata maana mpya bila ya niya ya kutukana mtu, cheo, au jinsiya. Je kuna mshikamano baina ya lugha hii ya kimaharajani na uvutiyo wa lugha yenyewe? Abdilatif Abdalla alipokuwa akielezeya nini ushairi alisema, "...vipande hivyo [vina] viwe vimetandwa na maneno ya mkato maalum na yenye lugha nyoofu, tamu na laini, lugha ambayo ni tetelezi kwa ulimi kwa kuitamka, lugha ambayo ina uzito wa fikra, tamu kwa mdomo wa kuisema, tumbuizi kwa masikio ya kuisikia na yenye kuathiri moyo uliokusudiwa na kama ulivyokusudiwa". Kwa

mintarafu wa donroo hili yaweza kuwa matumizi ya lugha ya SJA yanaafiki ushairi waliyouzoweya Waswahili na lugha tamu inayoandamana na maficho.

SJA amewatweza wanaume na wanawake, mashekhe wenzake, wazee katika jamii mpaka amemteremsha Mtume Muhammad kutoka cheo cha utume, mtukufu mwenye daraja ya juu kabisa katika umma wa Kiislamu, na kumfanya mume katika nyumba yake. Amekejeli tabiya ya wanaume na wanawake kufwata dini sana kutoka makazini, majumbani mpaka kitanrani na kusahau majukumu yao muhimu ya unyumba wao. Ametumiya maneno na misemo yenye hisiya na athari za kingono katika majukwaa yote bila ya kujali waliyohudhuriya. Lau si uhuru na uwazi uliyomo katika muktadha huu wa kimaharajani unaompa nafasi ya kujieleza atakavo bila sheriya za usemaji, basi SJA angehukumika amekufuru kwa kukiuka urasmi wa kishekhe wa Kiislamu. Ili kuchungwa asije akaiteka hadhira yake sana mpaka wakajisahau kwa kufurahishwa na hutuba basi kulikuwa na mwingiliyo wa 'Allahu Akbar' katika darasa moja (NN 1b) ili kupunguza uchekeshaji wa ziada.

SJA anaiga sauti za wanawake wavivu, vijana wasojuwa kuenresha nyumba zao, na wanaume mibabe wanaotambaza mamlaka katika nyumba zao. Piya, anafanya drama kwenye jukwaa la kumbi na mimbari za sehemu alizoalikwa na kucheka kwa kufurahi analolifanya. Darasa zake zina ukariri wa jambo, maswali ya balagha, anavuta nadhari ya hadhira na anatumiya kimya ili yale anayoyasema yasikizwe na yatiliwe maanani. Yote ameyafanya ili avutiye darasa zake na piya ujumbe wake uwafikiye hadhira bila kukasirikiyana wala kukoseyana heshima.

Darasa za Kiislamu na za SJA, hali kadhalika, huchota mawazo yake kutoka vitabu va kidini ya Kiislamu na maneno na mwenenro wa Mtume Muhammad ili kuwafunza waliyohudhuriya. Hii nriyo njiya ya mafunrisho katika Uislamu lakini SJA anatumiya vitabu hivi kwa uchache wa kiutangulizi tu. Anatiya sherehe nyingi na maelezo marefu kutokana na tajiriba zake za maishani binafsi na ofisini mwake anamoletewa mashitaka ya unyumba. Kwa kufanya hivi, SJA anavunja kaida ya mafunzo ya dini kwa kutumiya tajiriba zake zaidi kuliko kutumiya chimbo za *Kuruani*, maneno ya Mtume Muhammad, kauli ya pamoja ya wanazuwoni, na kisiyo lake kuhusu mambo ya unyumba kama mahali pa kupata ithibati ya maneno anayozungumziya. Jambo lingine ni kwamba darasa zenyewe hazianzi zikakamilika kwa kipinri kilichowekwa bali wakati huisha na yeye hajamaliza; kuna wakati (NN 1b) ilibidi akatizwe hutuba yake kutokana na muda.

Kama tulivoeleza katika sifa za umaharajani kwamba tamasha hili la maharajani lina muda wa kuwako linapokwisha muda wake nalo huisha. Darasa za SJA zimedhihirisha muda huu wa maisha yake. Anapoanza darasa mpaka anapofikiya sehemu kabla ya kuulizwa maswali kutoka kwa waliyohudhuriya vichekesho, dhihaka, mizaha na kila aina ya furaha hujitokeza. Wakati inapoanza sehemu ya kusikiza maswali na yeye mwenyewe kuyajibu mandhari hugeuka kuwa ya kutuna na jawabu hazina maelezo marefu na hutolewa kulingana na sheriya ya Kiislamu inavosema. Kutokana na 'kufa' kwa umaharajani wakati wa maswali tunabakiya kumwangaliya SJA kama nriye yule hapo kabla alikuwa akichekesha watu na kusema maneno hayo machafu. Fasili tuloipata sisi kuhusu matumizi ya maneno machafu ni kwa sababu tunapotumiya maneno haya huwa tunatusi uovu uliyoko katika jamii bila kujali kaida za kiutawala na husaidiya kuhuisha mwenenro mpya tena mzuri utakaofaa wanajamii wote; nriyo asili ya maharajani na umaharajani (Holquist, 1981). Hapa nripo tunapouona ule uhalisiya usiyoeleweka kwamba SJA ni kungwi, nyakanga, au ni shekhe? Sibina kwamba anwani ya makala haya imeshikanisha majina yote matatu kwa mtu mmoja. Ama ni mtu mwengine asiyeeleweka ni nani? Je, darasa zake za unyumba zenye umaharajani ni mwelekeo mpya SJA anaotaka ufwatwe ili lengo la kurakibisha jamii lifikiwe?

## HITIMISHO

Makala haya yalikuwa na lengo la kudhihirisha darasa za kimaharajani anazotumiya SJA ili kufikiliza ujumbe kwa umma wa Kiislamu. Darasa za unyumba ambazo zimemleteya yeye umaarufu Afrika Mashariki kwa Waislamu na wasiyokuwa Waislamu hali kadhalika. Ni darasa za kimaharajani kwamba zina mionroko ya kitamasha zenye miigo ya kidrama kuliko kuwa ni darasa za kutolewa na shekhe kwenye mimbari ya msikitini.

Umaharajani huu una sifa ya kuweka kanro kaida na miko ya kiusemaji rasmi katika muktadha maalumu. Maneno yanayotumiwa katika maharajani hayachungi sarufi, semantiki wala hayatilii maanani tasifida wakati wa kusemwa kwake. Mionroko ya kijamii huchekelewa, hudhihakiwa na kukosolewa na watu wasiyokuwa katika mamlaka ili jamii iweze kutowa dhiki ilizonazo na piya watawala waweze kujuwa makosa yao yako wapi na watadhibiti wapi katika jamii hiyo.

Data yetu ambayo imekusanywa kutoka kanra za nyakaninga za SJA zilizomo katika mtanrao wa youtube.com zilitupa sifa hizi za kimaharajani. Maneno machafu, misemo, matenro, na sauti za msemaji nrivo vigezo va data yetu tulivovitafiti katika kanra hizo. Uchanganuzi wetu wa kanra hizo umefaulu kupata data hiyo kwa kuiweka kwenye mkabala wa anayoyasema SJA na mionroko rasmi ya shekhe wa Kiislamu. Kwa kufanya hivo, tumeweza kupata data inayodhihirisha tafauti iliyopo baina ya kaida rasmi za shekhe wa Kiislamu na mionroko anayotumiya SJA kuwasilisha ujumbe wake.

Hatimaye, tunajiuliza kwa kugeuza hali kuwa juu-chini-chini-juu au kinyume-mbele kama kweli ujumbe wa SJA umefika kwa wanaosikiliza darasa zake za kimaharajani ambazo zimemleteya umaarufu Afrika Mashariki. Haya tunaweza kukisiya tu katika taarifa zilizoandikwa katika sehemu ya maoni ya kanra hizo katika mtanrao wa youtube.com ijapokuwa ufanisi wa darasa zenyewe na ufaafu wake haukuwa katika upeo wa makala haya. Utafiti mwengine ufanywe kuhusu asili, athari na ufaafu wa hutuba hizi za kimaharajani katika mafunzo, jumuiya ya Kiislamu na umma mzima wa Afrika Mashariki.

## MAREJELEO


Abulquasem, M. (1979). *Al Ghazali on Islamic guidance*. Malaysia.

Ali, A. H. T. (2013). *Taashira na utendaji katika nyimbo za harusi za Waswahili kisiwani Zanzibar*. Tasnifu ya Uzamivu (Haijachapishwa), Egerton University, Njoro.

Bachu, N. (2013, Juni 10) Haki za mume na mke 2 [video file]. Imetolewa: https://www.youtube.com/watch?v=5c-lEq2EKfA

Bachu, N. (2013, Juni 11) Haki za mume na mke 1 [video file]. Imetolewa: https://www.youtube.com/watch?v=J-76Ng5zWwM

Bernstein, M. A. (1983). When the carnival turns bitter: Preliminary reflections upon the abject hero. *Critical Inquiry*, *10*(2), 283-305.

Cory, H. (1947). Jando. Part I: The Constitution and Organization of the Jando. Katika *The Journal of the Royal Anthropological Institute of Great Britain and Ireland 77*(2), 159-168.

Cory, H. (1948). Jando: Part II: The Ceremonies and Teachings of the Jando. Katika *The Journal of the Royal Anthropological Institute of Great Britain and Ireland 78* (1/2), 81-94.

Cuddon, J. A. (1999). *The Penguin dictionary of literary terms and literary theory*. London: Penguin Books.

Draz, M. A. (2008). *The moral world of the Qur'an*. London: I.B. Tauris.

Fair, L. (1996). Identity, Difference, and Dance: Female Initiation in Zanzibar, 1890 to 1930. Katika *Frontiers: A Journal of Women Studies 17* (3), 146-172.

Finnegan, R. (2012). *Oral literature in Africa*. Cambridge: Open Books Publishers.

Ghazali, A. H. (1993). *Imam al Ghazali's Ihya ulum al din*. Karachi: Darul Ishaat.

Gray, J. (1992). *Men are from mars women are from venus: The classic guide to understanding the opposite sex*. Harper Collins e-books.

Holquist, M. (mh.). (1981). *M. M. Bakhtin: The dialogic imagination*. Austin: The University of Texas Press.

Kabira, W. M. (1983). *The Oral Artist*. Nairobi: East African Educational Publishers.

Krapf, L. (1882). *A dictionary of Suahili language*. London: Trubner & Co.

Lodhi, A. Y. & Westerlund, D. (1997). *African Islam in Tanzania*. Imechukuliwa http://www.islamtanzania.org/articles/islam2.htm Imesomwa 15/5/2018.

Mahmoud, M. A. (2004). *Utenzi wa ramani ya maisha ya ndoa (mke)*. Lamu.

Mahmoud, M. A. (2004). *Utenzi wa ramani ya maisha ya ndoa (mume)*. Lamu.

Morris, P. (1994). *The Bakhtin reader: Selected writings of Bakhtin, Medvedev and Voloshinov*. London: Edward Arnold (Publishers) Ltd.

Morson, G. S. (ed.).(1986). *Bakhtin: Essays and dialogues on his work*. Chicago: The University of Chicago Press.

Mwamzandi, I. Y. (2002). *Usemezano katika umalenga wa Kiswahili: Mfano wa taarab*. Tasnifu Shahada ya Uzamifu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Egerton, Njoro.

Nafzawi, U. M. (1886). *The perfumed garden of the Cheikh Nefzaoui: A manual of Arabian erotology*. Cosmopoli : for the Kama Shastra Society of London and Benares.

Nawawi, A. Y. S. (h.t.). *Riyadhu saliheen: The paradise of the pious*.

Senkoro, F. E. M. K. (1988). *Ushairi: Nadharia na tahakiki*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Shariff, I. N. (1988). *Tungo zetu: Msingi wa mashairi na tungo nyinginezo*. New Jersey: The Red Sea Press.

Shariff, I. N. (1991). Islam and secularity in Swahili literature: An overview. Katika K. W. Harrow (mh.) (1991) *Faces of Islam in African literature* (37-58). Portsmouth: Heinamann Educational Books.

Wamitila, K. W. (2003). *Kamusi ya fasihi: Istilahi na nadharia*. Nairobi: Focus Books.

**KIAMBATISHO 1**

Nyakaninga (NN) zilizotumiwa na kurejelewa katika makala haya:

NN 1b Sheikh juma amir tz https://www.youtube.com/watch?v=h_MXJeB5-uI Misk ya Roho | Ndoa | Sheikh juma Amir

NN 2 https://www.youtube.com/watch?v=bBsr0YL48m0 Aina 7 Za Wanawake Wabaya Part 1

NN 2b https://www.youtube.com/watch?v=IbV2Km53Qlw JUMA AMIR TABIA ZA WANAUME WA WABAYA

NN 3b https://www.youtube.com/watch?v=G371fvOoVkI Him and Her (Mke na Mme) [Swahili] | Sheikh Juma Amir | Journey of Faith Kenya 2017

NN 3bb https://www.youtube.com/watch?v=H6BtVG74ork 002 3 NASSOR BACHU LADHA 99 ALIZOPEWA MKE KATIKA TENDO LA NDOA

NN 4 https://www.youtube.com/watch?v=WUv1Yi9lCIA JUMA AMIR...ADABU ZA KITANDANI

NN 5 https://www.youtube.com/watch?v=dSweH38UQr8 Aina 7 Za Wanawake Wabaya Part 2

NN 5b https://www.youtube.com/watch?v=qcPRp7YgaJI Miujiza ya Allah-Sheikh Juma Amir

NN 6 https://www.youtube.com/watch?v=a3MN1s4H8Xw Aina 7 Za Wanawake Wabaya Part 3

NN 6b https://www.youtube.com/watch?v=KIQWSTtwV_I JUMA AMIR....SIFA ZA WANAUME 11 PART 1